

## Kukusanya mate kwa ajili ya kupima Covid-19

### Vifaa vya Kisanduku wa Ukusanyaji:

- Tyubu ya 5 mL iliyo na kifuniko cha skrubu
- Faneli
- Tishu zenye Alkoholi
- Mfuko wa biohazard
- Kifaa kinachoweza kunyonya



### Hatua za Kukusanya Mate:

1. Usile au kunywa kwa dakika kwa 30 kabla ya ukusanyaji wa sampuli.
2. Kwa matokeo bora, suuza kinywa chako na maji dakika 10 kabla ya kukusanya ili kuondoa chakula au uchafu mwingine.
3. Ondoa kifuniko na uweke funeli ndani ya tyubu ya kukusanya.
4. Tema mate kwa upole kupitia funeli hadi ndani ya tyubu ya kukusanya hadi ijazwe kwenye mstari mwekundu, bila kujumuisha mapovu yoyote yanayotokea juu.
5. Kumbusho: huu ni ukusanyaji wa mate ya kawaida; kupiga chafya na kukohoa kikohozi zaidi lazima kuepukwe.
6. Ikiwa unapata wakati mgumu kujaza tyubu, ifunge tyubu na uchukue dakika chache upumzike na kisha kukusanya mate zaidi kwenye mdomo kabla ya kujaribu tena.
7. Hakikisha hakuna vitu vingine isipokuwa ni mate vinavyokusanywa (kama makamasi au chembe za mabaki ya chakula) kwani hii inaweza kufanya sampuli yako kukataliwa na maabara.
8. Ondoa faneli na uitupe. Weka kifuniko kwenye tyubu na uikaze kuhakikisha haitavuja wakati wa usafiri.
9. Kwa usufi wa alkoholi uliopewa, safisha kabisa nje ya tyubu.
10. Andika jina la mwanafunzi na siku yake ya kuzaliwa kwenye tyubu ya vipimo kisha ubandike mojawapo ya misimbo pau iliyojumuishwa kwa tyubu, hakikisha kwamba msimbo pau haujafunika jina.
11. Weka tyubu ya mate iliyofunika kwenye mfuko wa biohazard uliopewa kisha uipeleke kwenye eneo la kisanduku cha barua cha shule yako siku ifaayo.
12. RNA ya virusi iliyo kwenye mate itabaki thabiti kwenye joto la kawaida au kwenye jokofu kwa angalau siku 7.



**Kuna maswali kuhusu Mpango wa Uchunguzi wa K-12, ukusanyaji wa mate, LabDash au ukaguzi wa Mate?**

**Tafadhali piga simu 503-769- 3234 ili kusungumza na maabara ya SCoPE.**

## Jinsi ya Kukusanya Sampuli katika LabDash

Mara tu unapokusanya sampuli, lazima ujisajili kwa LabDash KABLA ya kuipeleka kwenye eneo la shule yako ya kuacha.

**Ingia katika akaunti yako ya LabDash iliyoundwa hapo awali kwa Labdash.net**

### Hatua ya 1: Utambulishi wa Mgonjwa

- Katika kona ya juu kushoto ya skrini, chagua "Kusanya Sampuli"
- Chagua mgonjwa aliye sahihi kutoka kwa orodha uliyopewa na uchague "Kusanya"
- Kwenye skrini inayofuata, chagua tena mgonjwa sahihi na uchague "Inayofuata"

### Hatua ya 2: Sampuli ya Msimbo Pau

- Kwenye ukurasa wa Sampuli ya Msimbo pau:
  - Ikiwa unatumia kifaa cha mkononi, chagua "Scan Sampuli ya msimbo pau" na ufanye scan ya msimbo pau

AU

- Ikiwa unaingiza wewe mwenyewe, chagua "Ingiza Sampuli ya Msimbo pau" na uweke msimbo pau kwa mkono
- Chagua kitufe cha "Thibitisha" kilicho chini ya ukurasa

### Hatua ya 3: Kusanya Taarifa

- Chini ya Mtoa Agizo chagua "Dr. Melissa Sutton, MD, MPH"
  - Chini ya Aina ya Kipimo chagua "Covid-19"
  - Chini ya Njia ya kukusanya chagua "Mate"
  - Chini ya Jinsi Kipimo hiki Kitasimamiwa chagua :
    - "Bima" ikiwa uliingiza bima katika Labdash.
- AU
- "Huna bima" ikiwa haukingiza bima katika Labdash
  - **Bima yako HAITALIPISHWA na HUTAPOKEA bili ya hiki kipimo!**
- Jaza Orodha ya Dalili na taarifa zinazofaa
  - Chagua Thibitisha

### Hatua ya 4: Kagua na Uwasilish

- Thibitisha msimbo pau uliuingiza unalingana na msimbo pau ambao uko kwenye sampuli
- Weka sampuli lebo kwa jina la mwanafunzi na tarehe ya kuzaliwa

**Kuna maswali kuhusu Mpango wa Uchunguzi wa K-12, ukusanyaji wa mate, LabDash au ukaguzi wa Mate?**

**Vist [scopemolecular.org](http://scopemolecular.org) or call 503-769- 3234 to speak to the SCoPE Laboratory.**